FUNZO LA 38

1. Je, Waisraeli walipokosa maji, walimwamini Mungu awape maji?
-La.

2. Je, Waisraeli walipaswa kufanya nini iwapo hakukuwa na maji?
-Walipaswa kumuomba Mungu awape maji.

3. Je, Mungu alimuamuru Musa afanye nini ili wapate maji?
-Mungu alimuamuru Musa anene na mwamba.

4. Je, Mungu alimuamuru Musa afanye nini ili apate maji?
-Mungu alimuamuru Musa anene na mwamba.

5. Je, Mungu aliwaadhibu vipi Musa na Haruni?
-Mungu aliwaambia kuwa hawataingia katika nchi ya Kanaani.

6. Je, kwa sababu Waisraeli walizidi kulalamika, Mungu aliwafanyia nini?
-Mungu aliwaadhibu Waisraeli kwa kutuma nyoka wengi na wenye sumu miongoni mwao.

7. Je, dhambi inafananaje na hao nyoka?
-Kama vile nyoka walivyowauma watu na wakafa, ndivyo dhambi huuma watu na wanakufa.

8. Je, Mungu alimwambia Musa afanye nini ili awaokoe Waisraeli?



-Atengeneze nyoka wa shaba na amuangike juu ya mti.

9. Je, iwapo Waisraeli lazima waokolewe, wangefanya nini?
-Wamwangalie nyoka wa shaba aliyeinuliwa mtini.

10. Je, Waisraeli waliomwangalia yule nyoka wa shaba mtini, waliishi?
-Ndiyo.

11. Je, yule nyoka wa shaba alikuwa na uwezo wa kuwaokoa Waisraeli?
-La.

12. Je, ni nani pekee aliyekuwa na uwezo wa kuwaokoa Waisraeli?
-Mungu.

13. Je, dhambi ya Waisraeli ilistahili kifo?
-Ndiyo.

14. Je, ingawaje dhambi ya Waisraeli ilistahili kifo, Mungu aliwafanyia nini Waisraeli waliomtazama nyoka?
-Mungu aliwaokoa.

-Kwa sababu Waisraeli hawakumwamini Mungu, hawakuweza kuingia Kanaani.

-Kwa sababu Waisraeli hawakumwamini Mungu, walizunguka jangwani kwa miaka arubaini hadi watu wote wazima wakafa.

-Je, kwa nini Mungu aliwaadhibu Waisraeli?

-Kwa sababu walikataa kuamini Neno la Mungu ambalo Musa aliwaletea.

-Kama vile Musa alivyowaletea Waisraeli Neno la Mungu, ndivyo pia mimi nawaletea Neno la Mungu.

-Iwapo utakuwa kama Waisraeli na ukatae kuamini Neno la Mungu, basi pia utaadhibiwa na Mungu kama Waisraeli.

-Baada ya miaka arubaini, baada ya watu wote wazima kufa, Mungu aliwaongoza Waisraeli hadi kwa mpaka wa Kanaani.

-Kwa sababu Musa hakumtii Mungu, Mungu hakumruhusu kuwaongoza Waisraeli kuingia Kanaani.

-Kwa sababu Mungu hakumkubalia Musa kuwaongoza Waisraeli kuingia Kanaani, Musa alimchagua mtu mwingine kuwaongoza Waisraeli.

Tusome Hesabu 27:18-20 & 22-23

18-Bwana akamwambia Musa, Mtwae Yoshua, mwana wa Nuni, mtu mwenye roho ndani yake, ukamwekee mkono wako;

19-kisha ukamweke mbele ya Eleazari kuhani, na mbele ya mkutano wote; ukampe mausia mbele ya macho yao.

20-Nawe utaweka juu yake sehemu ya heshima yako, ili mkutano wote wa wana wa Israeli wapate kutii.



22-Musa akafanya kama Bwana alivyomwamuru; akamtwaa Yoshua, akamweka mbele ya Eleazari kuhani, na mbele ya mkutano wote;

23-kisha akaweka mikono yake juu yake, akampa mausia, kama Bwana alivyosema kwa mkono wa Musa.

-Je, kiongozi mpya aliyechaguliwa na Mungu badala ya Musa ni nani?
-Yoshua.

-Baada ya Yoshua kuwa kiongozi mpya wa Israeli, Mungu alimwambia Musa apande juu ya mlima uliokuwa karibu na mpaka wa Kanaani.

-Katika huo mlima, Mungu alimwonyesha Musa nchi ya Kanaani ambayo aliahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo.

Tusome Kumbu Kumbu la Torati 34:1-4

1-Musa akapanda kutoka uwanda wa Moabu mpaka mlima Nebo, hata kilele cha Pisga kukabili Yeriko. Bwana akamwonyesha nchi yote ya Gileadi hata Dani;

2-na Naftali yote, na nchi ya Efraimu na Manase, na nchi yote ya Yuda, mpaka bahari ya magharibi;

3-na Negebu, na uwanja wa bonde la Yeriko, mji wa mitende, hata mpaka Soari.

4-Bwana akamwambia, Hii ndiyo nchi niliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, nikisema, Nitawapa wazao wako. Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko.

-Kwa sababu Musa hakumtii Mungu, Mungu hakumruhusu aingie nchi ya Kanaani.

-Je, Mungu alitimiza Neno lake kwa kutomruhusu Musa kuingia Kanaani?
-Ndiyo.

-Mungu kamwe hutimiza Neno lake.

-Kamwe Mungu havunji Neno lake.

-Baada ya Mungu kumwonyesha Musa nchi ya Kanaani juu ya mlima, Musa akafa.

Tusome Kumbu Kumbu la Torati 34:5

5-Basi Musa, mtumishi wa Bwana, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana.

-Baada ya Musa kufa, Mungu alinena na Yoshua.

-Mungu alimwambia Yoshua kuwa ajiandae kuingia katika nchi ya Kanaani.

Tusome Yoshua 1:1-2

1-Ikawa baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa Bwana, Bwana akamwambia Yoshua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema,



2-Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli.

-Baada ya Musa kufa, Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuingia nchi ya Kanaani.

-Je, Mungu alitimiza ahadi yake na kuwapa uzao wa Ibrahamu nchi ya Kanaani?
-Ndiyo.

-Kama vile Mungu alivyowaahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo, aliwapa Waisraeli nchi ya Kanaani.

-Shetani na Farao walijaribu kuweka Waisraeli katika kifungo kule Misri.

-Lakini Mungu akatimiza ahadi yake ya kuwapa Israeli nchi ya Kanaani.

-Waisraeli hawakuamini kuwa Mungu angewapa maji na chakula jangwani.

-Lakini Mungu akatimiza ahadi yake ya kuwapa Israeli nchi ya Kanaani.

-Mungu kamwe hutimiza ahadi zake.
-Mungu kamwe hawezi vunja hata ahadi yake ata moja.

Tusome Yoshua 11:23a

23-Basi Yoshua akaitwaa hiyo nchi yote, sawasawa na hayo yote Bwana aliyokuwa amemwambia Musa;

-Waisraeli sasa waliishi katika nchi ya Kanaani.

-Pindi Yoshua alipokuwa hai, Waisraeli walimkumbuka Mungu.

Tusome Waamuzi 2:7

7-Watu hao wakamtumikia Bwana siku zote za Yoshua, na siku zote za hao wazee walioendelea siku zao baada ya Yoshua, hao waliokuwa wameiona hiyo kazi kubwa ya Bwana yote, aliyokuwa ameitenda kwa ajili ya Israeli.

-Baada ya muda, Yoshua alizeeka na akafa.

Tusome Waamuzi 2:8-9

8-Kisha Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Bwana, akafa, naye alipata umri wa miaka mia na kumi.
9-Nao wakamzika katika mpaka wa urithi wake katika Timnath-heresi, katika nchi ya vilima vilima ya Efraimu, upande wa kaskazini wa mlima wa Gaashi.

-Pindi Yoshua alipokuwa hai, Waisraeli walimkumbuka Mungu.

-Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli walifanya nini?



Tusome Waamuzi 2:10-13

10-Tena watu wote wa kizazi hicho nao walikusanywa waende kwa baba zao; kikainuka kizazi kingine nyuma yao, ambacho hakikumjua Bwana, wala hawakuijua hiyo kazi ambayo alikuwa ameitenda kwa ajili ya Israeli.
11-Wana wa Israeli walifanya yaliyokuwa ni maovu mbele za macho ya Bwana, nao wakawatumikia Mabaali.
12-Wakamwacha Bwana, Mungu wa baba zao, aliyewaleta kutoka katika nchi ya Misri, wakafuata miungu mingine, baadhi ya miungu ya watu wale waliokaa karibu nao pande zote, wakajiinamisha mbele yao; wakamkasirisha Bwana, akaghadhibika.
13-Wakamwacha Bwana, wakamtumikia Baali na Maashtorethi.

-Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli walimkataa Mungu na wakawa waovu sana.

-Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli walijifanyia mifano na kuiabudu badala ya Mungu.

-Watu waliokuwa majirani wa Israeli kule Kanaani waliabudu mifano iitwayo Baali na Ashtorethi.

-Kwa sababu Waisraeli walimkataa Mungu, pia wao waliabudu mifano ya Baali na Ashtorethi.

-Je, ni nani aliyewadanganya Waisraeli hadi wakamkataa Mungu na kuabudu mifano?

-Shetani.

-Shetani aliwadanganya watu, na watu wakadhani kuwa wanamwabudu Mungu.

-Lakini watu hawakuwa wanamwabudu Mungu.

-Watu walikuwa wanamwabudu Shetani aliyejificha kwa mifano ya Baali na Ashtorethi.

-Kama vile Shetani alivyojificha kwa nyoka ili awadanganye Adamu na Hawa, ndivyo alivyojificha kwa mifano ya Baali na Ashtorethi ili kuwadanganya watu.

-Shetani pia hujificha nyuma ya maroho na roho za mababu.

-Watu hudhani kuwa wanapoabudu maroho na roho za mababu kuwa wanamwabudu Mungu.

-Lakini hawamwabudu Mungu ila Shetani.

-Je, tunapoabudu kitu kingine isipokuwa Mungu, tunamwabudu nani?
-Shetani.

-Je, kwa nini Shetani anawaongoza watu kuabudu mifano?

-Kwa sababu Shetani anamchukia Mungu na hataki mtu yeyote amwabudu Mungu.



-Kwa sababu Shetani anawachukia watu wote na hataki mtu yeyote aokolewe na Mungu.

-Je, Mungu alijua kuwa Waisraeli waliabudu mifano ya Baali na Ashtorethi?
-Ndiyo.

-Je, Mungu alikasirishwa na Waisraeli kwa kuabudu mifano ya Baali na Ashtorethi?
-Ndiyo.

-Je, Mungu aliwafanyia nini Waisraeli?

Tusome Waamuzi 2:14-15

14-Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, naye akawatia katika mikono ya watu waliowateka nyara, akawauza na kuwatia katika mikono ya adui zao pande zote; hata wasiweze tena kusimama mbele ya adui zao.
15-Kila walikokwenda mkono wa Bwana ulikuwa juu yao kuwatenda mabaya, kama Bwana alivyosema, na kama Bwana alivyowaapia; nao wakafadhaika sana.

-Kwa sababu Waisraeli hawakumwabudu Mungu, ila mifano ya Baali na Ashtorethi, Mungu aliwaadhibu.

-Je, Mungu aliwaadhibu vipi Waisraeli kwa kuabudu mifano?

-Mungu aliwatuma adui wa Israeli kuharibu mimea ya Waisraeli.

-Mungu aliwatuma adui wa Israeli kuja na kuwaibia mifugo yao yote.

-Mungu aliwatuma adui wa Israeli kuja na kuwafanya Waisraeli watumwa wao.

-Je, Waisraeli walipotubu dhambi zao na kumwomba Mungu awasaidie, Mungu alifanya nini?

Tusome Waamuzi 2:16

16-Kisha Bwana akawainua waamuzi, waliowaokoa na mikono ya watu hao waliowateka nyara.

-Israeli walipotubu dhambi zao na kumwomba Mungu awasaidie, Mungu aliwachagua wanaume na wanawake ambao aliwatumia kuwaongoza Waisraeli kuwashinda adui zao.

-Je, hao wanaume na wanawake ambao Mungu aliwachagua kuwaongoza Waisraeli kuwashinda adui zao waliitwaje?

-Waamuzi.

-Pindi muamuzi aliyechaguliwa na Mungu alikuwa hai, Waisraeli walimfuata Mungu.

-Lakini muamuzi aliyechaguliwa na Mungu alipokufa, Waisraeli walirejea kuabudu mifano.

Tusome Waamuzi 2:17-19



17-Lakini hawakuwasikiliza hao waamuzi wao, maana walifanya uasherati kwa kuifuata miungu mingine, wakajiinamisha mbele yao; wakageuka upesi, na kuiacha njia ile waliyoiendea baba zao, waliozitii amri za Bwana bali wao hawakufanya hivyo.

18-Na wakati Bwana alipowainulia waamuzi, ndipo Bwana alikuwa pamoja na mwamuzi huyo, akawaokoa na mikono ya adui zao siku zote za mwamuzi huyo; maana Bwana alighairi kwa ajili ya kuugua kwao kwa sababu ya watu wale waliowaonea na kuwasumbua.

19-Lakini ikawa, wakati alipokufa mwamuzi huyo, wakarudi nyuma wakafanya maovu kuliko baba zao, kwa kuifuata miungu mingine ili kuitumikia, na kuinama mbele yao; hawakuacha matendo yao, wala njia zao za ukaidi.

-Ingawaje Mungu aliwaadhibu Waisraeli kwa dhambi yao, bado aliwapenda na aliwalinda.

-Je, kwa nini Mungu aliwapenda na kuwalinda Waisraeli?

-Kwa sababu Mungu aliahidi Abrahamu, Isaka na Yakobo kuwa uzao wao utakuwa mwingi na utakuwa taifa kubwa.

-Kwa sababu Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi kupitia kwa uzao wa Waisraeli.

-Kwa sababu Mungu aliahidi kutuma ujumbe wake, Biblia, kupitia kwa uzao wa Waisraeli.

-Mungu anawataka watu wote wasikie ujumbe wake ili waokolewe.

-Je, muamuzi wa mwisho wa Iraeli alikuwa nani?
-Samueli.

-Samueli alikuwa muamuzi wa Israeli kwa miaka mingi.

-Samueli alipozeeka, hakuna aliyechukua nafasi yake, kwa sababu wana wake hawakumwamini Mungu.

Tusome 1 Samueli 8:1-3

1-Hata Samweli alipokuwa mzee, aliwafanya wanawe wawe waamuzi juu ya Israeli.
2-Na jina la mwanawe mzaliwa wa kwanza aliitwa Yoeli; na jina la wa pili Abiya; walikuwa waamuzi katika Beer-sheba.
3-Ila wanawe hawakuenda katika njia zake, bali waliziacha, ili wapate faida; wakapokea rushwa, na kupotosha hukumu.

-Kwa sababu Samueli alizeeka na hakukuwa na wa kuchukua nafasi yake, Waisraeli walikusanyika na kwenda kumtembelea Samueli.

Tusome 1 Samueli 8:4-6

4-Ndipo wazee wote wa Israeli wakakutana pamoja, wakamwendea Samweli huko Rama;



5-wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako; basi, tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote.
6-Lakini neno hilo likawa baya machoni pa Samweli, waliposema, Tupe mfalme atuamue. Naye Samweli akamwomba Bwana.

-Kabla ya Samueli kufa, Waisraeli walimwambia afanye nini?

-Waisraeli walimwomba Samueli awachagulie mfalme awaongoze.

-Je, kwa nini hii ilimhuzunisha Samueli?

-Samueli alihuzunika kwa sababu Israeli ilimkataa Mungu kuwa mfalme wao.

-Je, ni nani aliyekuwa mfalme wa Israeli walipokombolewa kutoka Misri?
-Mungu.

-Je, ni nani aliyekuwa mfalme wa Israeli walipoongozwa jangwani?
-Mungu.

-Je, ni nani aliyekuwa mfalme wa Israeli walipopewa maji na chakula jangwani?
-Mungu.

-Je, ni nani aliyekuwa mfalme wa Israeli walipopewa nchi ya Kanaani?

-Mungu.

-Kwa miaka mingi, Mungu alikuwa mfalme wa Israeli.

-Tangu walipokombolewa kutoka kwa utumwa Misri, Mungu alikuwa mfalme wao.

-Lakini sasa, Waisraeli hawakumtaka Mungu awe mfalme wao.

-Waisraeli walitaka wawe kama jirani zao waovu, wawe na mfalme mwanadamu.

-Waisraeli walimkataa Mungu kama mfalme wao.

-Hivi ndivyo Mungu alivyomwambia Samueli:

Tusome 1 Samueli 8:7-8a

7-Bwana akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao.
8-Kwa kadiri ya matendo yote waliyonitenda tokea siku ile nilipowatoa katika Misri hata leo, kwa kuniacha mimi, na kwa kutumikia miungu mingine,

-Je, Mungu alimwambia nini Samueli?



-Mungu alimwambia Samueli kuwa Waisraeli hawakumkataa Samueli.

-Mungu alimwambia Samueli kuwa, kwa sababu Waisraeli walitaka mfalme, walimkataa Mungu awe mfalme wao.

-Je, Mungu aliwapa Waisraeli mfalme?

Tusome 1 Samueli 11:14-15

14-Kisha Samweli akawaambia watu, Haya! Na twendeni mpaka Gilgali, ili tuuimarishe ufalme huko mara ya pili.
15-Nao watu wote wakaenda Gilgali; wakamtawaza Sauli mbele za Bwana huko Gilgali; wakachinja sadaka za amani mbele za Bwana; na huko Sauli na watu wote wa Israeli wakafurahi sana.

-Ingawaje Waisraeli walimkataa Mungu awe mfalme wao, Mungu aliwapa mfalme mwingine.

-Jina lake ni Sauli.

-Sauli alikuwa mfalme wa kwanza mwanadamu wa Israeli.